# UTUJIBU

PATTY MWESIGA




TAFAKARI.

Ee Mwenyezi Mungu vitazame vilio vya wajane, nao wote wautafutao uso wako, Uwape mwangaza na nguvu ya kuvumilia hata wasikate tamaa katika kukutafuta wewe.

Uwajalie moyo wa kishujaa wale wote wanaotangaza neno lako ulimwenguni, nasi sote utufanye kuwa watoto wema kwa msaada wa mama yetu Bikira Maria tuwe washindi huko Mbinguni.

Tunakuomba utujalie kuishi vema maisha ya Ukristo, pia utushushie nguvu kiimani ili tuweze kuyashinda majaribu ya shetani, maana ulisema wewe ni nuru ya ulimwengu na kamwe humwachi mtu taabuni, pia wewe utawafadhili wote wakutafutao na kuyatii maneno yako ili waurithi ufalme wa milele.

Tunawaombea Maaskofu wetu, Mapadre, Watawa na Wanakwaya wote wadumu daima katika miito yao.

Tunawaombea na marehemu wote Ewe mwenyezi Mungu uliye mwingi wa rehema uziweke roho zao mahali pema peponi

PATTY MWESIGA
pattymwesiga88@gmail.com
+255762049842